

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA
Barua zote ziandikwe kwa: Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,



Simu Na 023 2402738,
Fax Na 023 402706
Unapojibu tafadhali taja:

S.L.P. 10,
MKURANGA,
PWANI.

Kumb. Na. LD/MK/6556/29

1/3/2021

✓ Mkurugenzi Mkuu,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P.938,
Dar es salaam

**YAH: KUITAMBULISHA KAMPUNI YA KNAUF GYPSUM TANZANIA LTD
KUNUNUA KIWANJA NA.25-27 KITALU 'B' KISEMVULE, WILAYA YA
MKURANGA**

Rejea mada tajwa hapo juu.


Ninakujulisha kwamba, Kampuni ya **Knauf Gypsum Tanzania Limited** ni Kampuni yenye kumilikiwa kwa hisa ambapo wamiliki wenye hisa nyingi ni Raia wa nje ya nchi. Kampuni hii imenunua viwanja Na.25-27 Kitalu 'B' Kisemvule, Wilaya ya Mkuranga kutoka Kampuni ya **Lodhia Steel Industries Limited** ambao miliki hii imesajiliwa kwa Na. PWN:4534

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999, fungu la 19-20 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na.26 ya mwaka 1997, aidha kwa kuzingatia fungu la 12 na 179 Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Tangazo la Serikali Na.72 la tarehe 4/5/2001, kanuni za Ardhi za 2001, kanuni ya 9C(v), kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

Halmashauri ya Wilaya inaitambulisha Kampuni hii kutoka nje ya nchi ili iweze kupatiwa Certificate of Incentive iliyofanyiwa marekebisho kwa kuonyesha kiwanja Na.25-27 Kitalu 'B' Kisemvule ili kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya **kukamilisha uhamisho wa miliki iliyouzwa** na kuandaa **Designation for Investment-Land form Na.1** ili viwanja hivi vigawiwe katika **kamati ya Ugawaji wa Ardhi Taifa** na hatimaye kutangazwa kuwa vya Uwekezaji katika Gazeti la Serikali.

Ninaambatanisha ramani ya upimaji, sale Agreement, Resolution minutes, MoU and Article of Association, Valuation Report, hati ya usajili wa Kampuni, uthibitisho wa Uraia wa wamiliki wa Kampuni, taarifa za kina za Kampuni na Original Certificate of Incentives inatarajiwa kurekebisha na kuingiza viwanja hivi vipya.

Naomba kuwasilisha kwako kwa hatua zaidi,


Chagiye R.M
Kny.Mkurugenzi Mtendaji (W),
Mkuranga

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W)
Mkuranga -Kwa taarifa

Knauf Gypsum Tanzania Limited
Dar es salaam -Fuatilia nyaraka husika TIC na uziwasilishe ili kukamilisha kazi.